**MAOMBI YA UDHAMINI**

# Utangulizi

Napenda kukuletea fursa ya kipekee ya kibiashara na kijamii kupitia **JUKANYE International History Festival 2026**—tamasha kubwa la kihistoria, kitamaduni na kibiashara linalotarajiwa kufanyika jijini Arusha nchini Tanzania kuanzia tarehe 01 - 13, September 2026, likishirikisha viongozi, wasanii, watafiti, watalii na washiriki kutoka ndani na nje ya Afrika.

Tamasha hili litaangazia urithi wa **viongozi wakuu wa ukombozi wa Afrika**, kwa kushirikisha **maonyesho, mijadala ya kitaaluma, filamu, muziki, michezo ya asili, kongamano la vijana, na matembezi ya kihistoria (Utalii)**.
Zaidi ya **watu 100,000** wanatarajiwa kuhudhuria moja kwa moja, na mamilioni kufuatilia kupitia runinga, redio na mitandao ya kijamii.

Tumeandaa vifurushi vya **udhamini** vyenye viwango tofauti vya bajeti kulingana na malengo ya biashara:

Tunaomba kukutana na ofisi yako ili tujadili namna bora kwa taasisi yako kushirikiana nasi katika tukio hili lenye thamani kubwa na faida kwa pande zote. Wasiliana nasi kwa mawasiliano yetu yanayopatikana katika tovuti hii.

**JUKANYE International History Festival 2026** si tukio la kawaida—ni jukwaa la kitaifa na kimataifa linaloleta pamoja historia, utamaduni, biashara na diplomasia ya kiuchumi. Kwa udhamini au ushiriki, biashara hupata nafasi ya kipekee kujitangaza, kuimarisha chapa, kushirikiana na wadau wakubwa, na kugusa hisia za mamilioni ya watu kupitia urithi wa viongozi wakuu wa Afrika na harakati za ukombozi. Huu ni uwekezaji wenye thamani ya kibiashara, kijamii na kisiasa.

# Aina za Udhamini kwa JUKANYE International History Festival 2026

| Aina ya Udhamini | Maelezo | Faida za Moja kwa Moja kwa Mdhamini |
|---|---|---|
| **1. Udhamini wa Fedha (Financial Sponsorship)** | Kampuni au taasisi huchangia kiasi cha fedha kusaidia maandalizi na utekelezaji wa tamasha | - Nembo na jina kuonekana kwenye mabango, mabasi, na vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa- Kipaumbele cha kutajwa kwenye matangazo na hotuba- Nafasi ya kuwa mtoa rasmi wa bidhaa/huduma kwa wageni na wageni mashuhuri |
| **2. Udhamini wa Bidhaa/Huduma (In-Kind Sponsorship)** | Kampuni huchangia bidhaa au huduma badala ya fedha, mfano: vyakula, vinywaji, vifaa vya mawasiliano, usafiri, vifaa vya jukwaa | - Kuonyesha bidhaa moja kwa moja kwa maelfu ya washiriki- Fursa za majaribio ya bidhaa (product sampling)- Ushirikiano wa kibiashara na washiriki wa ndani na wa kimataifa |
| **3. Udhamini wa Pamoja (Co-Sponsorship)** | Makampuni mawili au zaidi kushirikiana kudhamini tukio fulani maalum ndani ya tamasha, kama jukwaa kuu au maonesho ya sanaa | - Gharama zinagawanywa na faida za matangazo zinagawanywa- Nafasi ya kushirikiana na majina makubwa kwenye sekta nyingine- Taswira ya mshikamano na maendeleo ya jamii |
| **4. Udhamini wa Sekta Maalum (Sector-Specific Sponsorship)** | Mdhamini anakua mtoaji pekee wa bidhaa/huduma fulani kwa wageni wa tamasha, mfano: "Mdhamini Pekee wa Maji Rasmi" | - Umiliki wa kipekee wa soko ndani ya tamasha- Ushindani mdogo wa moja kwa moja- Uthibitisho wa chapa kama kiongozi wa sekta |

# Aina za Biashara Zinazoweza Kunufaika kwa Kudhamini au Kushiriki JUKANYE International History Festival 2026

| Sekta | Ujumbe kwa Sekta | Faida za Udhamini/Ushiriki |
|---|---|---|
| **1. Chakula na Vinywaji** (viwanda, migahawa, catering) | Nafasi ya kusambaza bidhaa moja kwa moja kwa maelfu ya wageni kupitia mabanda, mabango na matangazo ya moja kwa moja. | Kuongeza mauzo na kuimarisha chapa inayohusishwa na mshikamano wa Afrika. |
| **2. Utalii na Hoteli** (hoteli, mawakala wa usafiri, vivutio) | Huvutia watalii wa ndani na nje, kutoa nafasi ya kujitangaza na kuongeza mauzo. | Kuongeza wageni, mapato na kutambulika kimataifa. |
| **3. Sanaa na Utamaduni** (filamu, muziki, vitabu) | Fursa ya kuuza kazi za sanaa na kuonyesha utambulisho wa kitamaduni. | Kupanua soko na kujenga ushawishi wa kitamaduni. |
| **4. Benki na Huduma za Kifedha** (mabenki, bima, mikopo) | Fursa ya kuhudumia biashara na wageni wa tamasha kama mshirika wa fedha. | Kujenga imani na kuimarisha chapa kupitia uwajibikaji wa kijamii. |
| **5. Mawasiliano na Teknolojia** (simu, intaneti, IT) | Kuonekana kama kinara wa uvumbuzi na mtoa huduma rasmi wa kidijitali. | Matangazo makubwa na kuimarisha soko la teknolojia. |
| **6. Vifaa vya Ujenzi** (saruji, bati, rangi, maduka) | Kushiriki kwenye ujenzi wa majukwaa, mabanda na miundombinu. | Kuuza bidhaa kwa miradi ya muda na kudumu; matangazo ya kudumu. |
| **7. Usafirishaji** (mabasi, ndege, taxi, mizigo) | Kutoa huduma kwa washiriki na kuweka chapa kwenye vyombo vya usafiri. | Kuongeza abiria/wateja na matangazo ya moja kwa moja. |
| **8. Habari na Vyombo vya Habari** (TV, radio, magazeti, online) | Fursa ya kurusha matangazo ya moja kwa moja na vipindi maalum. | Kuongeza watazamaji/wasomaji na ushawishi wa chapa. |
| **9. Nishati** (mafuta, gesi, umeme, mbadala) | Kuwa mtoa nguvu rasmi wa tamasha na kuonyesha teknolojia za nishati. | Kutambulika kama kinara wa maendeleo endelevu na kufikia wateja wapya. |
| **10. Elimu na Mafunzo** (vyuo, shule, vituo) | Kushiriki kwenye kongamano na warsha za vijana. | Kuongeza uandikishaji na kujihusisha na mijadala ya kitaaluma. |
| **11. Afya na Lishe** (hospitali, kliniki, vifaa, lishe) | Kutoa huduma na kampeni za afya kwa hadhira kubwa. | Kuwafikia maelfu kwa huduma na elimu ya afya. |
| **12. NGO’s na Mashirika ya Maendeleo** (ya ndani/kimataifa) | Kuonyesha miradi na matokeo yake kwa hadhira pana. | Kujenga mtandao wa ushirikiano na kuimarisha taswira ya taasisi. |